**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**15 Mei, 2025**
**Kigoma.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**
**UZINDUZI WA MRADI WA KUJENGA UWEZO WA KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI KATIKA MAZINGIRA YA MKOA WA KIGOMA, TANZANIA**

---

**Ndugu Wanahabari,**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR) inatekeleza na kuratibu shughuli za Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira hapa nchini kwa manufaa mapana ya Kitaifa kwa Kizazi hiki na kizazi kijacho. Utekelezaji wa shughuli za Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira zinafanywa kwa mujibu wa mwongozo wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura Namba 191.

**Ndugu Wanahabari,**

Kwa msingi huo, katika utekelezaji wa shughuli hizi, Serikali imekuwa ikitekeleza majukumu yake Kitaifa na Kimataifa ambapo katika nyanja za Kimataifa Serikali ni mwanachama wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya Mazingira (*Multilateral Environmental Agreements – MEAs*) na Kikanda ikiwemo Mkataba wa Umoja wa

Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi *(United Nations Framework Convention on Climate Change-UNFCCC)* ambao ilisaini tarehe 12 Juni 1992 na kuridhia tarehe 17 Aprili 1996. Lengo la Mkataba huu ni kupunguza ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ikolojia ya dunia katika kiwango ambacho kitapunguza mrundikano wa gesijoto zitokanazo na shughuli za kibinadamu ili kutoathiri mifumo ikolojia ikiwemo; mfumo ya hali ya hewa na uzalishaji wa chakula duniani ili kuhakikisha maendeleo endelevu duniani.

**Ndugu Wanahabari,**

Kupitia Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund - GCF) unaoratibiwa chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNCHR) kwa ufadhili unaotolewa kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) inatarajia kuanza utekelezaji wa mradi wa "**Kujenga Uwezo wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Mazingira ya Mkoa wa Kigoma".** Mradi huo utatekelezwa katika wilaya tatu za mkoa wa Kigoma ambazo ni Wilaya ya Kasulu, Kibondo na Kakonko.

**Ndugu Wanahabari,**

Mradi huo unafadhiliwa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF) kwa thamani ya kiasi cha jumla ya Dola za Kimarekani milioni 19 sawa na fedha za kitanzania kiasi cha takriban shilingi bilioni 26,975,000,000 na unatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka huu 2025 hadi 2030. Lengo la mradi ni kujenga uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania mahsusi katika mkoa wa Kigoma.  Uzinduzi huu umekuja wakati ambapo nchi ipo katika machakato wa kuzindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambapo katika masuala muhimu yaliyopewa

kipaumbele ni masuala ya hifadhi ya mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ambayo yamebainishwa katika Nguzo ya Tatu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**Ndugu Wanahabari**,

Mradi huu wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika mazingira ya Mkoa wa Kigoma, utakuwa moja ya miradi mikubwa ya mfano, unaotumia mbinu zinazozingatia hifadhi ya mifumo ikolojia kama moja ya mkakati muhimu wa kujenga ustahimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo yenye changamoto kubwa za kimazingira na migogoro hasa katika kwa jamii za wakimbizi na wakazi wanaozunguka kambi za wakimbizi za Nyarugusu, Nduta na Mtendeli zilizopo katika Wilaya ya Kasulu, Kibondo na Kakonko katika mkoa wa Kigoma ambapo mradi unatarajiwa kutekelezwa moja kwa moja katika Wilaya hizo chini ya Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

**Ndugu Wanahabari**,

Kwa sasa, mkoa wa Kigoma una wakazi takriban milioni 2.3 na wakimbizi 250,000 zaidi kutoka nchi jirani, ambao wengi wao wanaishi katika kambi za wakimbizi za Nduta na Nyarugusu. Kigoma ni mkoa wenye wakazi milioni 2.3 na eneo la kilomita za mraba 37,000, ukihifadhi wakimbizi 280,000 kutoka nchi jirani katika kambi za Nduta, Mtendeli na Nyarugusu, makazi ambayo yalianzishwa haraka kushughulikia mahitaji muhimu ya kibinadamu. Aidha, takriban asilimia 90 ya jamii zinazowapokea katika maeneo yanayozunguka kambi za wakimbizi na idadi kubwa ya wakimbizi wanajihusisha na kilimo, ufugaji na uvuvi, ambavyo ni shughuli na huduma zinazotegemea mfumo wa ikolojia wa eneo hilo. Walakini, vichochezi vya hali ya hewa na visivyo vya hali ya hewa vimechagia kuharibu zaidi mifumo hii ya ikolojia.

**Ndugu Wanahabari**,

Kati ya 2011 na 2018, Kigoma ilipoteza asilimia 5.3 ya eneo la misitu, sawa na hekta 108,000 za misitu, kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi kama vile kuongezeka kwa matukio ya moto, mvua na mafuriko, na kuongezeka kwa joto na hatari kama vile mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa rasilimali za maji kwa muda mrefu na uharibifu wa ardhi kwa muda mrefu. Hivyo, Mradi unaoenda kuzinduliwa katika mkoa wa Kigoma utanufaisha moja kwa moja zaidi ya watu takribani 570,000 na kurejesha takriban hekta 42,000 za misitu na mazingira ya ikolojia ya kilimo ili kusaidia maisha ya wenyeji katika eneo la mradi. Mipango ya matumizi bora ya ardhi inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, misitu, kilimo, maji, udhibiti wa mafuriko na hatua za kisera zitatekelezwa kwa mbinu jumuishi.

**Ndugu Wanahabari**,

Uzinduzi wa mradi unatarajiwa kufanyika tarehe 15 Mei, 2025 na kufuatiwa na Kikao cha Kamati ya Usimamizi wa Mradi kitakachofanyika tarehe 16 Mei 2025 katika ukumbi wa Kigoma Social Hall, uliopo Manispaa ya Kigoma – Ujiji mkoa wa Kigoma. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Y. Masauni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu (Mazingira na Muungano).

**Ndugu Wanahabari**,

Warsha ya uzinduzi wa Mradi huo, inatarajiwa kuhudhuriwa na wadau mbalimbali, ikiwemo Viongozi kutoka Mkoa wa Kigoma na Wilaya zinazotarajiwa kutekeleza mradi; Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kigoma; Viongozi kutoka katika Wizara, Taasisi na Idara za Serikali; Wataalamu na Maafisa Waandamizi kutoka Serikalini, Wakuu na Wawakilishi wa Mashirika ya Umoja wa mataifa na Washirika wa Maendeleo; Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa na Kitaifa;  Asasi za Kiraia; Wawakilishi wa Jumuiya za Wakimbizi na Vyombo mbalimbali vya Habari.

**Ndugu Wanahabari,**

Kabla ya kuhitimisha taarifa hii, napenda kuwashukuru ninyi Wanahabari kwa kuitikia wito katika siku hii ya leo lakini pia kwa jitihada mnazofanya katika kuhabarisha umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi. Kama mnavyofahamu, Mabadiliko ya Tabianchi ni changamoto kubwa hivi sasa duniani na inaathiri mazingira, ukuaji wa uchumi, maendeleo ya jamii na usalama wa viumbe wote duniani. Hivyo, Ni matumaini yangu kuwa mtaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA…!!**